

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA  
NJOMBE**

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na: NDC/S.50/18/VOL.II/30

Tarehe: 16/09/2022

## **TANGAZO**

**MWALIKO WA ZABUNI**

**ZABUNI NA. LGA/031/2022/2023/NC/01**

**UPANGISHAJI WA ENEO KWA AJILI YA UZALISHAJI  
KOKOTO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe natoa mwaliko kwa Wafanyabiashara wa kokoto na wale wenye uwezo wa kupangishwa eneo la uzalishaji wa kokoto lenye ukubwa wa ekari 4.28kuomba Zabuni hii.

Eneo la uchimbaji wa kokoto lipo Nyalive kijiji cha Matiganjola Kata ya Ikuna Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Muombaji anakaribishwa kutembelea eneo hilo kwa gharama zake. Zabuni inatangazwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Zabuni hii ni ya muda wa miaka 7 ambayo itakuwa ikihuishwa kila baada ya mwaka mmoja

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inamiliki Leseni ya eneo hilo yenye namba PML 000431NJB(Primary Mining Licence) iliyotolewa na Wizara ya Madini.

### **MASHARTI YA MWOMBAJI:**

1. Iwapo ni mtu binafsi muombaji awe ni raia Tanzania mwenye umri zaidi ya miaka 18 na kuendelea

2. Iwapo ni kampuni muombaji awe ni kampuni ambayo inaundwa na raia wa Tanzania pekee, wakurugenzi wake wote ni wa raia wa Tanzania na usimamizi wa kampuni hiyo uwe unafanywa moja kwa moja au siyo moja kwa moja hapa Tanzania na Watanzania
3. Iwapo ni ubia uwe umeundwa na Watanzania pekee
4. Mwombaji awe tayari kulipa ada ya upangaji kwa kila mwezi, ambayo lazima aitaje kwenye maombi yake.
5. Muombaji aeleze kiasi cha mtaji ambao atawekeza katika uchimbaji kokoto
6. Muombaji aeleze gharama za uendeshaji atakazokuwa akitumia kuzalisha kokoto au malighafi zitokanazo na kokoto kwa kila mwezi
7. Muombaji aeleze gharama za uendeshaji atakazokuwa anatumia kwa kila mwezi
8. Muombaji awe tayari kuweka dhamana`` Bank Guarantee`` itakayolingana na thamani ya malipo ya ada ya pango kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kuanza kwa mkataba, ambayo itakuwa ikihuishwa kila baada ya mwaka mmoja.
9. Muombaji awe tayari kulipa ada ya upangaji kila baada ya miezi mitatu
10. Muombaji awe tayari kufanya tathmini ya athari za kimazingira(EIA) kabla ya kuanza kazi kwa gharama zake mwenyewe.
11. Muombaji aambatishe kwenye maombi yake nakala ya nyaraka muhimu ambazo ni:
  - Leseni ya Biashara
  - Cheti cha Usajiri wa kampuni
  - Cheti cha mlipa Kodi (TIN)
  - Taarifa za kifedha (Bank statement) ya hivi karibuni miezi miwili
  - Kampuni wasilishe 'Power of attorney'

